# Kutoka Katika Mbio Za Panya Hadi Katika Milango Ya Lulu

**na**

**Terry Warford**

# Kutoka Katika Mbio Za Panya Hadi Katika Milango Ya Lulu

**na**

**Terry Warford**

**Novemba 5, 2011**

# Kutoka Katika Mbio Za Panya Hadi Katika Milango Ya Lulu

Katika Math. 24:37-39, "*Kwa maana kama vile ilvyokuwa siku za Nuhu, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu. Kwa kuwa kama vile siku zile zilizokuwa kabla ya gharika watu walivyokuwa wakila na kunywa, wakioa na kuolewa, hata siku ile aliyoingia Nuhu katika safina, wasitambue hata gharika ikaja, ikawachukuwa wote, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu.*"

Tunatambua kwamba Mungu aliangamiza dunia kwa Gharika kwa sababu ya kutokutii kwa mwanadamu na machafuko. Lakini hususan katika kifungu kiki, Yesu alikuwa anatuonya kuhusu mambo tofauti tofauti juu ya kutokutii, hiyo ya kuendelea mara kwa mara katika maisha yetu ya kila siku bila Mungu. Hakuna chochote kibaya juu ya kula na kunywa, kuoa na kuolewa. Tunapaswa kula na kunywa ili tuishi. Tunaambiwa kwamba ndoa ni zawadi toka kwa Mungu. Kwa nyongeza, tunapaswa kwenda kazini kila siku ili kuzisaidia familia zetu, au katika shule kusoma. Lakini kama tukiendana na hisia za maisha yetu kila siku, bila kuiachia Yesu tuatjikuta wenyewe hatujajiandaa wakati akirudi.

Kitu kimoja ambacho kitatusaidia kila siku ni kufanya kazi hizi za kila siku katika njia inayompendeza Mungu. Katika kufanya hivyo, tunayageuza kutoka katika kufanya vitu katika ulimwengu pasipo Mungu kwenda katika huduma kwa yeye. Hivi vitu siyo vitu pekee tunazoweza kufanya kwa ajili ya Bwana kila siku. Lakini maranyingi zimekuwa zikidharauliwa, na ynaweza kubadilishwa kutoka katika kazi za kidunia hadi katika kazi za kiungu kimsingi katika badiliko la tabia. Ni wazo linalo furahisha, ambayo inaweza kubariki maisha yetu ya Ukristo.

Sasa tunawezaje kubadilisha maisha yetu ya kula na kunywa katika huduma kwa ajili ya Yesu? Yote ni katika tabia. Tunapata sehemu 3 katika badiliko la tabia.

Kwanza kabisa, kumbuka kwamba Baraka hizi zote hutoka kwa Mungu. Yakobo 1:17, "*Kila kutoa kuliko kwema na kila kitolewacho kilicho kamili, hutoka juu, hushuka kwa Baba wa mianga; kwake hakuna kubadilika, wala kivuli cha kugeuka geuka.*" Wafil. 4:19 inasema. "*Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu ndani ya Kristo Yesu.*"

Fuata hatua hiyo ya kwanza na kumwamini ili kutoa Baraka hizi, ili kwamba tuweze kutazamia mambo mengi ya kiroho. Math. 6:31-33, "*Msisumbuke, basi, mkisema, Tule nini? Au Tunywe nini? Au Tuvae nini.*

*Kwa maana hayo yote mataifa huyatafuta; kwa sababu Baba yenu wa mbinguni anajua ya kuwa mnahitaji hayo yote. Bali utafuteni kwa ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa.*" Usijali umuhimu wa maisha haya. Mwamini Mungu akupe. Zaburi 37:3, "*Umutumaini BWANA ukatende mema,ukae katika nchi, upendezwe na uaminifu.*"

Hatua nyingine ni shukrani kwa Baraka hizi ambazo Mungu anazotoa. Jenga tabia ya shukrani, kama tunavyosoma katika 1 Tim. 4:3-5. Andiko hili linahusu tabia ya kutoa shukrani hasa kwa viakula vyetu. Na tunahitaji sit u kutoa shukurani kwa Mungu, lakini pia kumuonyesha shukrani zetu katika maombi. Katika kifungu hiki Paulo alikuwa akionyesha baadhi ya mafundisho ya uongo. Moja lilikuwa linahusu vyakula vyetu. "*Wakiwazuia watu wasioe, na kuwaamuru wajiepushe na vyakula ambvyo Mungu aliviumba vipokewe kwa shukrani na walio na imani wenye kuijua hiyo kweli. Kwa maana kila kiumbe cha Mungu ni kizuri, wala hakuna cha kukataliwa, kama kikipokewa kwa shukrani; kwa kuwa kimetakaswa kwa neno la Mungu na kwa kuomba.*"

Tunaweza kula tu na kunywa kwa akili zetu popote pale, na tusifikirie Mungu na chakula kamwe. Au tunaweza kutazamia kwenye ladha na virutubisho vya chakula chetu, na kuonyesha ujuzi wake wenyewe kwa ajili yake. Au tunaweza kukumbuka kwamba chakula chetu hutoka kwa Mungu, tunamtegemea ili atupatie, tukishukuru kwalo na kuonyesha shukrani zetu kwa Mungu kwa maombi kupitia kwa jina la Yesu Kristo. Kufanya hivyo kila mara tunakula na kunywa inatuzaidia kumtazama Yesu siku nzima. Kufanya hivyo kunachukua kula na kunywa jukumu la kila siku ya kuwa na ujuzi katika sehemu ya huduma kwa Kristo. Ila tu kwa kurekebisha tabia.

Kitu cha pili ambacho Yesu alionyesha ni kuoa na kuolewa. Ndoa ni Baraka ambayo Mungu ametoa kwa wanadamu wote. Hutakiwi kuwa Mkristo ili uoe au uolewe. Waeb. 13:4 inasema, "*Ndoa na iheshimiwe na watu wote, na malazi yawe safi; kwa maana waasherati na wazinzi Mungu atawahukumia adhabu.*" Tunawezaje kugeza ndoa zetu kutoka katika matendo ya kila siku ya dunia hadi katika matendo ya Kristo?

Kwanza kabisa, kama ilivyo kwa chakula chetu, kumbuka kwamba ndoa zetu ni Baraka kutoka kwa Mungu. "*Uishi kwa fura pamoja na mke umpendaye, siku zote za maisha yako ya ubatili, ulizopewa chini ya jua; siku zote za ubatili wako, kwa maana huo ni sehemu yako ya maisha; na katika taabu zako ulizozitaabika chini ya jua.*" Na Mithali 18:22 inasema, "*Apataye mke apata kitu chema; naye ajipatia kibali kutoka kwa BWANA.*"

Hii inatuongoza tena katika kutoa shukrani. Waef. 5:20, "*Na kumshukuru Mungu Baba sikuzote kwa mambo yote katika jina la Bwana wetu Yesu Kristo.*" "*Mambo yote*" kimsingi inaweza kujumlisha ndoa na mwenza.

Fuatilia hii kwa kuishi katika ndoa zetu kama Mkristo anavyotakiwa. Tusiruhusu maisha ya kila siku yaharibu ndoa zetu kama jinsi ulimwengu unavyofanya. Weka jitihada, wajibika, kujitoa, msamaha, na upendo kama Mkristo anavyotakiwa kuwa, na kufanya hivyo kila siku. Waef. 5:24-25, "*Lakini kama vile kanisa limtiivyo Kristo vivyo hivyo wake nao wawatii waume zao katika kila jambo. Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda kanisa akajitoa kwa ajili yake.*" Tusiwapende wake zetu kama ulimwengu unavyo fanya. Umpende kama Kristo alivyolipenda kanisa! Wakol. 3:17 ni kifungu kinachojulikana, "*Na kila mfanyalo kwa neno au kwa tendo, fanyane yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye.*" Msitari miwili inayofuata inaonyesha agizo hili kwa ndoa zetu. Wakol. 3:18-19, "*Ninyi wake watiini waume zenu, kama ipendavyo katika Bwana. Ninyi waume, wapendeni wake zenu msiwe na uchungu nao.*"

Katika somo hili, pia tunataka kuangalia kazi zetu au shule. Tunafanya hivyo kwa sababu ya muda inayochukuwa katika siku yetu. Muda wa kazi wa kawaida ni masaa 8 kwa siku, au kwa haraka haraka robo tatu ya kila siku, siku 5 kwa wiki au zaidi. Nyingi ya kazi zetu zinahitaji zaidi ya muda kuliko hilo. Tena, tabia njema itabadilika masaa 8 ya mwendo wa panya katika masaa 8 ya kuweka hazina mbinguni. Hebu tuone jinsi gani.

Tena, inaanza kwa kutambua kwamba kazi yetu au shule ni Baraka kutoka kwa Mungu na kuwa na shukrani kwa ajili yake. 1 Wathes. 5: 18, "*Shukuruni kwa kila jambo, maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu.*"

Pili, tunatakiwa kuwa na uhakika kwamba tunafanya kazi kwa sababu sahihi. Hatupo katika maisha haya ili tuwe matajiri au tuwe na mali nyingi kwa ajili yetu sisi. Yesu alisema katika Luka 12:15, "*Akawaambia, angalieni, jilindeni na choyo, maana uzima wa mtu haumo katika wingi wa vitu vyake alivyo navyo.*"

Badala yake, malengo yetu ni kujitafutia, familia zetu na kuwa tayari kushirikiana na walio na mahitaji. Tunasoma katika 1 Wathes. 4:11-12 kwamba tunapaswa kujitafutia, "*Tena mjitahidi kutulia, na kutenda shughuli zenu, na kufanya kazi kwa mikono yenu wenyewe, kama tulivyowaagiza; ili mwenende kwa adabu mbele yao walio nje, wala msiwe na haja ya kitu chochote.*" Katika 1 Tim. 5:8 tunaona kwamba tunahitajika kuhudumia familia zetu, "*Lakini mtu yeyote asiyewatunza walio wake, yaani, wale wa nyumbani mwake hasa, ameikana imani tena ni mbaya kuliko mtu asiyeamini.*" Na katika Waef. 4:28 tunasoma kwamba tunahitajika kuwa wakarimu kwa wengine, "*Mwibaji asiibe tena; bali afadhali afanye juhudi, akitenda kazi iliyozuri kwa mikono yake mwenyewe apate kuwa na kitu cha kumgawia mhitaji.*

Alafu tunafunga badiliko la tabia zetu katika kazi zetu kwa kufanya kazi kama Yesu Kristo ndiye Mkuu wetu, (au mwalimu). Wakol. 3:22-24, "*Ninyi watumwa, watii hao ambao kwa mwili ni bwana zenu, katika mambo yote, si kwa utumwa wa macho kama wajipendekezao kwa wanadamu, bali kwa unyofu wa moyo, mkimcha Bwana. Lo lote mfanyalo, lifanyeni kwa moyo kama kwa Bwana, wala si kwa wanadamu, mkijua ya kuwa mtapokea kwa Bwana ujira wa urithi. Mnamtumikia Bwana Kristo.*"

Kwa hiyo tunabadilisha kula na kunywa katika kumtumikia Kristo kwa kutambua kwamba Baraka hizi utoka kwa Mungu, tukimtarajia kutupatia mahitaji ya maisha haya, kuwa na shukrani kwake yeye na kuonyesha shukrani zetu kwa maombi.

Tunabadilisha ndoa zetu kutoka katika hali ya uchungu hadi katika Ukristo tena kwa kutambua kuwa Baraka hizi hutoka kwa Mungu, kuwa na shukrani kwa njoa yetu na wenzetu, na kuishi kama Mkristo anavyo paswa kuishi. Kwa mfano, waume wapendeni wake zenu kama Kristo alivyolipenda kanisa.

Na tunabadilisha kazi zetu (au shule) katika huduma ya Ukristo tena kwa kutambua mabaraka za Mungu na kuwa na shukrani kwalo, kwa kufanya kazi kwa nia njema – siyo tama, bali kujitafutia wenyewe, familia zetu na kuwa tayari kuwasaidia wenzetu, na kwa kufanya kazi kama Yesu Kristo ndiye Mkuu wetu (au mwalimu).

Tunapofanya mabadiliko haya katika tabia, kumbuka tunageza shughuli hizi za kawaida katika huduma ya Kristo. Lakini pia tunajenga mazingira mazuri ya tabia, upendo na kutoa na roho ya shukrani. Hivyo hatua hizi pia zinabariki sehemu zingine za maisha ya Ukristo. Kimsingi zitafanya ndoa zetu na kazi zetu kuwa bora. Zaidi sana zinatusaidia kuweka juhudi katika mtazamo wetu mbali na mbio ya panya ya kuishi kila siku hadi katika kuishi kwa Kristo kuweza kuzawadiwa Siku ya Hukumu.

Wakol. 3:1-2, "*Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatufuteni yaliyo juu Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu. Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi.*"

Imetolewa kwa upendo wa Ukristo,

Ndg. Terry Warford